

DHIMA YA TAFSIRI KATIKA KUFANIKISHA UFUNDISHAJI WA ISIMU KATIKA VYUO
VIKUU

Silas Owala

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi

Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga Odinga cha Sayansi na Teknolojia-Kenya

Ikisiri

Ufundishaji wa isimu hutegemea tafiti ambazo zimefanywa katika sehemu mbalimbali ulimwenguni. Hii ni kwa sababu matokeo ya kiisimu hutokana na lugha hai mbalimbali zaidi ya elfu sita ambazo hupatikana duniani. Ili kuweza kuelewa yaliyomo katika matawi mbalimbali ya isimu kama vile fonolojia, mofolojia, semantiki na sintaksia, kuna haja ya wataalamu wanaofundisha isimu kusoma na kuelewa tafiti zilizofanywa katika lugha hizo. Matokeo ya tafiti hizo huwasilishwa katika lugha anuwai. Hali hii inazua haja ya kuipa tafsiri nafasi ya kufanya tafiti hizo ziweze kueleweka. Uhawilishaji wa matokeo ya tafiti hizo humsaidia anayefunza kuweza kuwasilisha dhana zilizomo katika lugha ambayo wanafunzi wake wanaweza kuelewa. Wanaofunza Kiswahili kwa mfano wanahitaji uwezo wa kutafsiri kutoka lugha mbalimbali ili kuweza kuboresha uwezo wao wa kufunza isimu. Baadhi ya vitabu ambavyo vinatumiwa na walimu wa Kiswahili navyo vimeandikwa katika lugha ya Kiingereza na lugha nyinginezo. Makala hii inaangazia hali ilivyo katika ufundishaji wa Isimu, vitabu vilivyopo na nyenzo nyingine pamoja na umuhimu wa uwezo wa tafsiri kama kifaa cha kufanikisha masomo ya isimu.